

REF: PPR/11- 2/11

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
TAREHE 21 NOVEMBA 2011**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei elekezi na bei kikomo za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 21 Novemba 2011**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Novemba 2011. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli zimeshuka, ambapo bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimepanda kidogo. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS (22.86)/lita sawa na asilimia (1.12); Dizeli imepanda kwa TZS 51.23/lita, sawa na asilimia 2.58 na Mafuta ya taa imepanda kwa TZS 46.45/lita, sawa na asilimia 2.35. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na kushuka kwa bei ya petroli katika soko la dunia na kupanda kwa bei ya dizeli na mafuta ya taa katika soko la dunia na pia kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani, (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS (22.86)/lita sawa na asilimia (1.16), Dizeli imepanda kwa TZS 51.23/lita, sawa na asilimia 2.67 na bei ya Mafuta ya Taa imepanda kwa TZS 46.45/lita, sawa na asilimia 2.44.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo la Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)
Dar es Salaam	2,020	2,034	2,021
Arusha	2,104	2,118	2,105
Arumeru	2,104	2,118	2,105
Karatu	2,122	2,137	2,124
Monduli	2,110	2,124	2,111
Ngorongoro (Loliondo)	2,181	2,195	2,182
Kibaha	2,025	2,039	2,026
Bagamoyo	2,031	2,045	2,032
Kisarawe	2,027	2,042	2,029
Mkuranga	2,030	2,044	2,031
Rufiji	2,048	2,062	2,049
Dodoma	2,079	2,093	2,080
Kondoa	2,111	2,125	2,112
Kongwa	2,076	2,090	2,077
Mpwapwa	2,080	2,094	2,081
Iringa	2,084	2,098	2,085
Kilolo	2,089	2,103	2,090
Ludewa	2,150	2,164	2,151
Makete	2,143	2,157	2,144
Mufindi	2,094	2,108	2,095
Njombe	2,113	2,127	2,114
Bukoba	2,235	2,249	2,236
Biharamulo	2,209	2,223	2,210
Chato	2,192	2,206	2,193
Karagwe	2,251	2,265	2,252
Muleba	2,226	2,240	2,227
Ngara	2,201	2,215	2,202
Misenyi	2,243	2,257	2,244
Kigoma	2,251	2,265	2,252
Kasulu	2,237	2,251	2,238
Kibondo	2,215	2,229	2,216
Moshi	2,094	2,108	2,095
Hai	2,097	2,111	2,098
Mwanga	2,087	2,101	2,088
Rombo	2,115	2,129	2,116
Same	2,080	2,094	2,081
Siha	2,100	2,114	2,102
Lindi	2,079	2,093	2,080

Kilwa Masoko	2,054	2,068	2,055
Liwale	2,100	2,114	2,101
Nachingwea	2,108	2,122	2,109
Ruangwa	2,106	2,120	2,107
Babati	2,142	2,156	2,143
Hanang	2,153	2,167	2,154
Kiteto	2,153	2,168	2,155
Mbulu	2,155	2,169	2,156
Simanjiro	2,174	2,188	2,175
Musoma	2,198	2,212	2,200
Bunda	2,190	2,204	2,191
Serengeti	2,244	2,258	2,245
Tarime	2,209	2,224	2,211
Mbeya	2,127	2,141	2,128
Chunya	2,137	2,151	2,138
Ileje	2,140	2,154	2,141
Kyela	2,143	2,157	2,144
Mbarali	2,111	2,125	2,112
Mbozi	2,136	2,150	2,138
Rungwe	2,136	2,150	2,137
Morogoro	2,045	2,059	2,046
Mikumi	2,061	2,075	2,062
Kilombero	2,083	2,097	2,084
Mahenge	2,093	2,107	2,094
Kilosa	2,063	2,077	2,064
Mvomero	2,055	2,069	2,056
Mtwara	2,093	2,107	2,094
Masasi	2,118	2,132	2,119
Newala	2,124	2,138	2,125
Tandahimba	2,117	2,131	2,118
Mwanza	2,170	2,184	2,171
Geita	2,211	2,225	2,212
Kwimba	2,206	2,220	2,207
Magu	2,178	2,192	2,179
Misungwi	2,176	2,190	2,177
Sengerema	2,202	2,216	2,203
Ukerewe	2,229	2,243	2,230
Sumbawanga	2,193	2,207	2,194
Mpanda	2,227	2,241	2,228
Nkasi	2,206	2,220	2,207
Songea	2,143	2,157	2,145
Mbinga	2,177	2,191	2,178
Namtumbo	2,172	2,186	2,173
Tunduru	2,202	2,216	2,203
Shinyanga	2,149	2,163	2,150

Kahama	2,162	2,177	2,164
Bukombe	2,175	2,189	2,176
Bariadi	2,190	2,204	2,191
Kishapu	2,177	2,191	2,178
Maswa	2,181	2,195	2,182
Meatu	2,188	2,202	2,189
Singida	2,111	2,125	2,112
Iramba	2,123	2,137	2,124
Manyoni	2,095	2,109	2,096
Tabora	2,174	2,188	2,175
Igunga	2,128	2,142	2,129
Nzega	2,139	2,153	2,140
Sikonge	2,186	2,200	2,187
Urambo	2,187	2,201	2,188
Tanga	2,066	2,080	2,067
Handeni	2,057	2,071	2,058
Kilindi	2,080	2,094	2,081
Korogwe	2,059	2,073	2,060
Lushoto	2,069	2,083	2,070
Mkinga	2,080	2,094	2,081
Muheza	2,066	2,080	2,067
Pangani	2,073	2,087	2,074

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	1,952.78	1,966.88	1,953.92

Haruna Masebu
MKURUGENZI MTENDAJI
EWURA